

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



TANGAZO

**YAH: UANDIKISHAJI WA VIJANA WA KUJIUNGA
NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT) KWA
UTARATIBU WA KUJITOLEA (HIARI)
MWAKA 2018/2019**

**OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MVOMERO INAWATANGAZIA
NAFASI ZA KUJIUNGA NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT) KWA
VIJANA WOTE WANAOPENDA KUJIUNGA KWA UTARATIBU WA
KUJITOLEA MWAKA 2018/2019.**

SIFA ZA MWOMBAJI:-

1. AWE RAIA WA TANZANIA

2. UMRI:-

- (A) KWA VIJANA WENYE ELIMU YA DARASA LA SABA (VII) UMRI KUENZIA MIAKA 16 HADI 18.**
- (B) VIJANA WENYE ELIMU YA KIDATO CHA NNE (IV) UMRI USIWE ZAIDI YA MIAKA 20.**
- (C) VIJANA WENYE ELIMU YA KIDATO CHA SITA (VI) UMRI USIWE ZAIDI YA MIAKA 22.**

- (D) VIJANA WENYE ELIMU YA STASHAHADA UMRI USIWE ZAIDI YA MIAKA **25**.
- (E) VIJANA WENYE ELIMU YA SHAHADA UMRI USIWE ZAIDI YA MIAKA **26**.
- (F) VIJANA WENYE ELIMU YA SHAHADA YA UZAMILI UMRI USIWE ZAIDI YA MIAKA **30**.
- (G) VIJANA WENYE ELIMU YA SHAHADA YA UZAMIVU UMRI USIWE ZAIDI YA MIAKA **35**.
3. MWOMBAJI AWE NA AFYA NJEMA, AKILI TIMAMU NA ASIWE NA ALAMA YEYOTE YA MICHORO MWILINI (**TATTOO**).
4. MWENYE TABIA NA NIDHAMU NZURI, HAJAPATIKANA NA HATIA MAHAKAMANI NA HAJAWAHI KUFUNGWA.
5. KWA VIJANA WALIOMALIZA ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA NNE (**IV**) WAVE WALIOMALIZA KUENZIA MWAKA **2016, 2017 NA 2018** WENYE UFAULU UFUATAO:-
- a) WAVE WAMEFAULU NA WAVE NA ALAMA (POINTS) ZISIZOPUNGUA 32.
- b) VIJANA KIDATO CHA SITA WAVE NA UFAULU WA DARAJA LA KWANZA HADI LA NNE.
6. AWE NA CHETI CHA ELIMU YA MSINGI ALIYEHITIMU DARASA LA SABA (**VII**).
7. AWE NA CHETI HALISI CHA KUZALIWA (**ORIGINAL BIRTH CERTIFICATE**).
8. AWE NA CHETI HALISI CHA KUMALIZA SHULE (**SCHOOL LEAVING CERTIFICATE**).
9. AWE NA CHETI HALISI CHA MATOKEO (**ORIGINAL ACADEMIC CERTIFICATE/TRANSCRIPT**).

10. ASIWE AMETUMIKIA JESHI LA POLISI, MAGEREZA, CHUO CHA MAFUNZO AU KMKM WALA KUAJIRIWA NA IDARA NYINGINE SERIKALINI.
11. ASIWE AMEPITIA JKT OPARESHENI ZA NYUMA.
12. ASIWE AMEJIHUSISHA NA MATUMIZI YA MADAWA YA KULEVYA, BANGI NA YANAYOFANANA NA HAYO.
13. KWA WALE WENYE VIPAJI VYA MICHEZO MBALIMBALI NA SANAA SIFA ZA ELIMU NI SAWA NA ZILIZOTAJWA HAPO JUU.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

1. BARUA ZA MAOMBI ZIPITISHWE NA WATENDAJI WA KATA NA VIJJI HUSIKA KUTHIBITISHA UKAZI WA MHUSIKA KATIKA ENEO HILO NA BARUA HIZO ZIAMBATANISHWE NA NAKALA YA VYETI VILIVYOAINISHWA HAPO JUU.
2. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYO NI TAREHE **14 JUNI, 2019** SAA **09:30 ALASIRI** SIKU YA **IJUMAA**.
3. USAILI UTAFAANYIKA TAREHE **18 NA 19 JUNI, 2019** SIKU YA **JUMANNE** NA **JUMATANO** KUANZIA SAA **03:00 ASUBUHI** KATIKA **UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA WILAYA MVOMERO** NA WAOMBAJI WOTE WALIOKIDHI MASHARTI TAJWA HAPO JUU WANATAKIWA KUFIKA NA VYETI HALISI (**ORIGINAL CERTIFICATE**).
4. OFISI YA MKUU WA WILAYA HAITAHUSIKA NA GHARAMA ZUZOTE ZITAKAZOJITOKEZA **MFANO: USAFIRI, CHAKULA, MALAZI** N.K.
5. UNAPOONA TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZIO.
6. BARUA ZA MAOMBI ZITUMWE KWA:-
MKUU WA WILAYA
S.L.P. 59
MVOMERO - MOROGORO.


MICHAEL A. MAGANGA
**KATIBU TAWALA WILAYA
MVOMERO
30/05/2019**